**KIDATO CHA TATU 2025**
**KARATASI YA KWANZA**
**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

**SWALI LA LAZIMA – SWALI LA KWANZA**
**BARUA RASMI**
**MUUNDO**

- Anwani ya mwandishi upande wa kulia,juu kabisa.
- Tarehe chini ya anwani ya mwandishi.
- Answani ya mwandikiwa/mlengwa pambizoni kushoto chini kidogo ya tarehe.
- Anza kwa cheo cha mwandikiwa katika anwani hiyo pamoja na anwani yake.
- Ruka msitari mmoja chii ya anwani hiyo,kisha andika maamkuzi/maamkizi.
- Chini ya maamkizi pawe na mada/mintarafu.

  **MINT: MIKAKATI YA KUIMARISHA MATOKEO YA SOMO LA KISWAHILI NCHINI.**

  - Sharti ikumbukwe kwamba kama anwani ya mwandishi ni ya mlazo,basi katika barua aya zote huanzia ndani kidogo,yaani hatua chache kutoka kwa msitari ulio pambizoni kushoto.
  - Aidha,iwapo anwani ni ya mlazo,basi hakuna kuruka mstari uanzapo aya mpya.
  - Iwapo anwani ni wima,mwili utaendelezwa kwa aya zinazobainishwa kwa kuruka msitari.
  - Na sharti anwani zote ziakifishwe ipasavyo.
  - Kimalizio sharti kiwepo.

    **Mfano**: Wako mwaminifu
    Sahihi
    Jina la mwandishi
    Cheo (iwapo kipo)
  - Kimalizio hiki huja upande wa kushoto anwani ikiwa wima au huwekwa upande wa kulia anwani ikiwa mlazo.

  **HOJA ZENYEWE(MAUDHUI)**

  - Vipindi kuongezwa.
  - Pawepo na walimu wa kutosha.
  - Vitabu vya kutosha.
  - Teknolojia mpya kushirikishwa kufunza Kiswahili.
  - Ushauri kuhusu mtazamo hasi eti Kiswahili ni kigumu.
  - Kubuniwa kwa Baraza la Lugha nchini ili kutoa mwelekeo kuhusu matumizi ya Kiswahili,uundaji msamiati,n.k.
  - Marekebisho kwa silabasi – ni pana sana kwa miaka mine.
  - Ushirikiano kuimarisha baina ya walimu na wanafunzi ili kukuza lugha ndani na nje ya darasa.
  - Kiswahili kutambulika kama lugha ya wenyeji/wakenya na ya kujivinia(uzalendo) – si mtihani tu.
  - Kuandaa makongamano zaidi baina ya shule mbalimbali.
  - Maktaba ya shule yawe na vitabu zaidi vya Kiswahili ,vya aina kadha na majarida yajae ili kuwapa motisha.
  - Mashindano ya uandishi wa insha.

    *Hakiki hoja zingine zitakazojitokeza.
    (tuza hoja zozote tano(5) zilizofafanuliwa vizuri au kwa kina)

**SWALI LA PILI**

- Ni swali la moja kwa moja linalohitaji mwanafunzi kueleza undani madhara/hasara au maangamizi ambayo yamesababishwa na mafuriko(mvua nyingi) hapa nchini.
- Pawe ne kichwa/anwani.
- Utangulizi – katika aya ya kwanza.

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes
Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes
©2015 Pyramid Consultants P.O BOX 67593-00200 Nairobi 0722614502/0733494581 / www.kcsetopical.co.ke

- Mwili – utakaoonyesha madhara ya mafuriko.
- Hitimisho.
  **TANBIHI** : katika mwili wa insha,ni sharti kila hoja ichukue aya yake huru.
  **Hoja zenyewe**
  - Kuharibiwa kwa barabara kwa kuwa teketeke.
  - Madaraja kubomoka.
  - Mimea kuoza – hivyo kutokua na mazao mema.
  - Nyumba na majengo mengine kuharibiwa.
  - Kukwamiza shughuli/kazi za kujitafutia riziki au za ujenzi wa taifa.
  - Kisingizio cha wengine kuzembea kazi.
  - Magonjwa kutokea.
  - Kiwango cha uchumi kuzorota – mavuno machache ukarabati mwingi wa miundo-msingi.
  - Kuzidisha umaskini.
  - Vifo vya watu,ndege na wanyama.
    (hoja zozote 5(tano)zilizoelezwa kikamilifu)

**SWALI LA TATU**
**RIPOTI RASMI**

**MUUNDO**
- Sura iwe ya ripoti rasmi.
- Pawe na kichwa chenye dhana zifuatazo:
  - kutaja shughuli yenyewe.
  - mahali
  - wakati /kipindimwaka

- Anza kwa kuandika nena'utangulizi'.
- Aya ya kwanza iwe ni utangulizi utakaojumuisha mambo yafuatayo:
  - taja ni nani aliyeagiza uchunguzi ufanywe.
  - kipindi cha kufanya uchunguzi na kuwasilisha ripoti.
  - kiini cha uchungizi huo.
  - taja majina ya wanajopo na vyeo vyao.

- Mwanafunzi aonyeshe mbinu za kusanya data.Aya hii huja baada ya utangulizi.
- Matokeo yafuate kama kijichwa kingine.Huu ndio mwili hasa wa ripoti unaobeba maudhui au hoja zitakikanazo.
- Kila hoja iwe na kijichwa chake au pawe na mada ndogo ndogo katika mzima wa ripoti tangu kichwa hadi mwisho.
- Pawe na mapendekezo.
- Hitimisho.
- Kimalizio kiwepo.Mfano
  Ripoti hii imekusanywa na kuandaliwa na,
  Sahihi
  Jina la mwandalizi/mwandishi.
  Cheo/wadhifa wa mwandishi.

4. Rais wa taifa lako amekuteua kuwa katibu wa jopo la watu sita ili kuchunguza dhima ya utandawazi ulimwenguni.
   Andaa ripoti.
   - Kusahihisha na kuboresha mawasiliano.
   - Kutoa huduma haraka kwa urahisi.
   - Kusaidia katika uvumbuzi.
   - Hukuza utangamano wa kimataifa.
   - Hukuza mashindano miongoni mwa mataifa mbalimbali katika sekta kadhaa.

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes
©2015 Pyramid Consultants P.O BOX 67593-00200 Nairobi 0722614502/0733494581 / www.kcsetopical.co.ke

- Inatoa ripoti kamilifu au tarakiiwimu kikamili.
- Muda mfupi – hakuna kupoteza wakati.
- Gharama kupungua.
- Hutumia nafasi /eneo dogo – haihitaji nafasi kubwa au pana.
-Kupunguza matumizi ya vitabu/Karatasi za kusomwa na kuandikwa.

**SWALI LA NNE**

- Ni mtungo wa kubuni.
- Mwanafunzi aandike kisa kitakachosimulia na kudhihirisha kuwa kwa kweli mwanamke anatoa mchango mkubwa katika kuiendeleza jamii.
- Hadithi ionyeshe namna mwanamke alivyo wa umuhimu katika jamii.
- Sharti pawe na kisa maalum au cha kipekee kuhusu mwanamke/msichana Fulani anayetambulika kwa jina na vitendo katika hadithi ya mwanafunzi.
- Mwanafunzi amalizie maneno /kifungu alichopewa bila kuzidisha wala kupunguza hata chembe.
- Atakayezidisha au kupunguza neno/maneno mbali na aliyopewa kama kimalizio achukuliwe kuwa alijitungiwa swali na kilijibu.
  Huyu atuzwe alama ya ‘D’ yaani maki 3.
- Sharti mwanafunzi adhihirishe ubunifu wake wa hali ya juu na matumizi wa msamiati.

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes
©2015 Pyramid Consultants P.O BOX 67593-00200 Nairobi 0722614502/0733494581 / www.kcsetopical.co.ke